Toleo 84 - Jumada II 1445 H / Januari 2024 M

Jarida la UQAB



# JE, PALESTINA
# TUTAIKOMBOA VIPI

# Enyi Watawala katika Ardhi za Waislamu ... Sikizeni na Muzingatie...

Kuna vita vya kikatili vinavyofanywa dhidi ya Gaza na kukosekana uingiliaji kati wa majeshi ya Waislamu, haswa yale yanayoizunguka Palestina, licha ya mauaji yote yanayofanywa na umbile la Kiyahudi, mchana na usiku. Vita hivi vya kikatili sasa vimeambatana na taarifa zinazofuatana kutoka kwa wakoloni wa makafiri, haswa Marekani na Uingereza, kuhusu suluhisho la dola mbili kwa Palestina. Suluhisho hili ni dola ya Mayahudi katika sehemu kubwa ya Palestina, na baadhi yake ni imeondolewa nguvu ya kijeshi ambayo Wapalestina wamehifadhiwa! Suluhisho hili limetajwa mara nyingi, midomoni mwa watawala katika ardhi za Waislamu, haswa nchi za Kiarabu zinazoizunguka Palestina, huku mamlaka ya Palestina ikiwa mstari wa mbele wa wito huu ...

Kisha, kukawa na mwendelezo wa uvamizi wa kikatili kwa karibu siku hamsini. Halafu, mkataba wa kusitisha vita wa wiki nzima uliidhinishwa na umbile la Mayahudi, kisha kuubatilisha, na kuendelea na hata ukatili mkubwa zaidi na bila ya uingiliaji kati wa majeshi. Yote haya ni kuonyesha kana kwamba umbile la Mayahudi ni nguvu kubwa, kiasi kwamba majeshi ya Waislamu hayawezi kupigana nao. Kwa hivyo, yote yanaleta mazingira ya kujadiliana nalo juu ya mradi muovu, suluhisho la dola mbili, ambalo ni usaliti kwa Mwenyezi Mungu, Mtume wake, na waumini.

**Enyi watawala katika Ardhi za Waislamu:**

Umbile la Kiyahudi sio watu wa vita na ushindi, badala yake ni kama Mwenyezi Mungu (swt) alivyosema,

لَنْ يَضُرُّوكُمْ إِلَّا أَذًى وَإِنْ يُقَاتِلُوكُمْ يُوَلُّوكُمُ الْأَدْبَارَ ثُمَّ لَا يُنْصَرُونَ

**"Maadui hawatakudhuruni ila ni maudhi tu. Na wakipigana nanyi watakupeni mgongo, na tena hawatanusuriwa."** [Surah Aali Imran 3:111]. Kama munavyoona, waumini wachanga wanapigana na Mayahudi, kwa idadi ndogo na uwezo mdogo kuliko umbile la Kiyahudi, na bado umbile hili halijafanikiwa ushindi mpaka wa leo. Kwa hivyo, ikiwa majeshi ya Waislamu yatasonga, sio hata majeshi yote ya Waislamu, bali yale tu yanaoizunguka Palestina, au hata baadhi yake, basi umbile la Kiyahudi halingebakia hata athari yake kuonekana.

Palestina ni ardhi ya Kiislamu .. Umar al-Farooq (ra) aliifungua .. Salahudin Al-Ayubi akaikomboa .. na Abdul Hameed II akailinda. Sio ya kuuzwa. Haikubali kugawanywa kati ya watu wake, na wale awanaoikalia kimabavu, kuwafukuza watu wake kutoka kwake. Suluhisho lake sio suluhisho la dola mbili. Badala yake, suluhisho lake ni kama Mwenyezi Mungu Al-Aziz, Al-Jabbar alivyosema, na maneno Yake (swt) ndio suluhisho la kweli,

وَاقْتُلُوهُمْ حَيْثُ ثَقِفْتُمُوهُمْ وَأَخْرِجُوهُمْ مِنْ حَيْثُ أَخْرَجُوكُمْ **"Na wauweni popote mwakutapo, na muwatoe popote walipo kutoeni."** [Surah Al-Baqarah 2:191].

**Enyi Watawala katika Ardhi za Waislamu:**

Je! Kuuwawa shahidi na kujeruhiwa kwa Waislamu elfu sitini huko Gaza haitoshi kwenu kuhamasisha majeshi kwa ajili ya kuwanusuru?! Mwenyezi Mungu (swt) amesema,

وَإِنِ اسْتَنْصَرُوكُمْ فِي الدِّينِ فَعَلَيْكُمُ النَّصْرُ **"Lakini wakiomba msaada kwenu katika Dini, basi ni juu yenu kuwasaidia."** [Surah Al-Anfal 8:72].

Je! Kelele za watoto wa Gaza, vilio vya kina mama, uchungu wa waliofiwa, na vilio vya wanaume na wanawake wakongwe, havitoshi kwenu, kuhamasisha majeshi, katika kuwanusuru?!!

Je! Muendelezo wa mauaji, kunyofolewa kwa miili, na miguu, ya mashahidi, na umwagaji damu ya mashahidi na majeruhi kutoka chini ya vifusi na magofu, haitoshi kwenu kuwanusuru watu wa Gaza?!!

Je! Hamuoni? Je! Hamusikii? Je! Damu haichemki mishipa mwenu, kiasi kwamba muinusuru Gaza Hashim?!!

Je! Hamuoni aibu mbele ya Mwenyezi Mungu, Mtume wake, na waumini, kiasi kwamba msikataa kutoa Nusrah (kuwanusuru)? Hakika, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema ukweli katika Hadith iliyopokewa na Al-Bukhari, ambaye alisema kwamba Adam alisimulia, kwamba Shu'bah kutoka kwa Mansour, ambaye alisema, nilimsikia Rab'i bin Hiraash akizungumza kutoka kwa Abu Masoud, kwamba Mtume (saw) amesema,

إِنَّ مِمَّا أَدْرَكَ النَّاسُ مِنْ كَلَامِ النُّبُوَّةِ إِذَا لَمْ تَسْتَحْيِ فَاصْنَعْ مَا شِئْتَ **"Hakika katika miongoni mwa waliyoyapata watu kutoka kwa maneno ya Mitume (as) ni, 'ikiwa huoni haya basi fanya unavyotaka.'"**

**Enyi Watawala katika Ardhi za Waislamu:**

Tunatambua kuwa uaminifu wenu kwa wakoloni wa makafiri, haswa Marekani, na utiifu wenu kwao ndio unaokuzuieni kuinusuru Gaza na watu wake ili kuhifadhi viti vyenu vibovu. Mumesahau, au mumejisahaulisha, kwamba kwa kufanya hivyo hamupotezi tu Akhera yenu,

***Endelea... UK 3***

munapoteza hata maisha ya dunia hii. Hakika, wakoloni makafiri watakutupeni kama konde za tende, na kuvunja viti vyenu, pindi wakimaliza kufikia malengo yao kupitia nyinyi. Kilichowatokea watangulizi wenu hapo awali, ni funzo kwenu, ikiwa tu mutatambua hilo.

Hakika, Mwenyezi Mungu Al-Qawwi, Al-Aziz, amesema kweli,

أَفَلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَتَكُونَ لَهُمْ قُلُوبٌ يَعْقِلُونَ بِهَا أَوْ آذَانٌ يَسْمَعُونَ بِهَا فَإِنَّهَا لَا تَعْمَى الْأَبْصَارُ وَلَكِنْ تَعْمَى الْقُلُوبُ الَّتِي فِي الصُّدُورِ

**“Je! Hawatembei katika ardhi ili wapate kuwa na nyoyo zao za kuzingatia, au masikio ya kusikilia? Kwani hakika si macho yanayo pofuka, lakini zinazo pofuka ni nyoyo ziliomo vifuani.”** [Surah Al-Hajj 22:46].

Enyi Askari katika Majeshi ya Waislamu:

Imekuwa takriban miezi miwili tangu uvamizi wa kikatili wa Mayahudi ulipoanza dhidi ya watu wenu huko Gaza ... na licha ya mauaji ambayo umbile la Kiyahudi limeyafanya, na bado wanayafanya, ambayo wanawake, watoto, 'ulema na wazee waliuawa shahidi ... na licha ya uharibifu wa nyumba, mahospitali, Misikiti na taasisi, watawala wanakuzuieni kuwanusuru ndugu zenu huko Gaza, mukikaa na kunyamaza kimya! Je! Hamuogopi kukaa tuli, kiasi kwamba Ghadhabu kutoka kwa Mola wenu (swt) iwashukie juu yenu?

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا مَا لَكُمْ إِذَا قِيلَ لَكُمُ انْفِرُوا فِي سَبِيلِ اللهِ اثَّاقَلْتُمْ إِلَى الْأَرْضِ] أَرَضِيتُمْ بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا مِنَ الْآخِرَةِ فَمَا مَتَاعُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا قَلِيلٌ * إِلَّا تَنْفِرُوا يُعَذِّبْكُمْ عَذَاباً أَلِيماً وَيَسْتَبْدِلْ قَوْماً غَيْرَكُمْ وَلَا تَضُرُّوهُ شَيْئاً وَاللَّهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

**“Enyi mlio amini! Mna nini mnapo ambiwa: Nendeni katika Njia ya Mwenyezi Mungu, mnajitia uzito katika ardhi? Je, mmeridhia maisha ya dunia kuliko ya Akhera? Lakini starehe za maisha ya dunia kulinganisha na ya Akhera ni chache (38). Kama hamwendi atakuadhibuni adhabu chungu, na atawaleta watu wengine, wala nyinyi hamtamdhuru chochote. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu (39).”** [Surah At-Tawbah 9:38-39].

Je, hamutamani moja ya matendo mema mawili [ushindi au shahada]?

يَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَيُدْخِلْكُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ وَمَسَاكِنَ طَيِّبَةً فِي جَنَّاتِ عَدْنٍ ذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ * وَأُخْرَى تُحِبُّونَهَا نَصْرٌ مِنَ اللهِ وَفَتْحٌ قَرِيبٌ وَبَشِّرِ الْمُؤْمِنِينَ

**“Atakusameheni dhambi zenu, na atakutieni katika Mabustani yapitiwayo na mito kati yake, na maskani nzuri nzuri katika Bustani za milele. Huko ndio kufuzu kukubwa. (12) Na kinginecho mkipendacho, nacho ni nusura itokayo kwa Mwenyezi Mungu, na ushindi ulio karibu! Na wabashirieni Waumini! (13).” [Surah As-Saf 61:12-13]. Je hamutamani hadhi katika dunia hii na kesho Akhera?**

**Enyi Askari katika Majeshi ya Waislamu:**

Kimbilieni kuwanusuru ndugu zenu huko Gaza. Endapo watawala watasimama dhidi yenu, basi wakamateni kwa kila njia inayowezekana. Wanusuruni ndugu zenu katika Ardhi Iliyobarikiwa, na mufanye kuwe ni kushindwa kukubwa kwa umbile la Mayahudi kama vile kulivyokuwa kushindwa kukubwa kwa Makruseda huko Al-Quds Ash-Sharif, na pia kushindwa kukubwa kwa Wamongolia huko Ain Jalut ... na hivyo Palestina irudi kwa ujumla wake, kuwa makaazi ya Uislamu, kama ilivyokuwa hapo awali. Itapambwa tena kwa bendera ya Rayah ya Khilafah, bendera ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), kwani ni ardhi ya Isra'a na Miraj ... Ardhi Iliyobarikiwa na vilivyobariki viunga vyake .

سُبْحَانَ الَّذِي أَسْرَى بِعَبْدِهِ لَيْلاً مِنَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ إِلَى الْمَسْجِدِ الْأَقْصَى الَّذِي بَارَكْنَا حَوْلَهُ لِنُرِيَهُ مِنْ آيَاتِنَا إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

**“SUBHANA, Ametakasika aliye mchukua mja wake usiku mmoja kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti wa Mbali, ambao tumevibariki vilivyo uzunguka, ili tumuonyeshe baadhi ya Ishara zetu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia na Mwenye kuona.”** [Surah Al-Israa 17:1].

Jitokezeni, Enyi Askari, muwanusuru ndugu zenu huko Gaza Hashim. Mnusuruni Mwenyezi Mungu (swt), Naye atakunusuruni.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنْ تَنْصُرُوا اللهَ يَنْصُرْكُمْ وَيُثَبِّتْ أَقْدَامَكُمْ * وَالَّذِينَ كَفَرُوا فَتَعْساً لَهُمْ وَأَضَلَّ أَعْمَالَهُمْ * ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ كَرِهُوا مَا أَنْزَلَ اللهُ فَأَحْبَطَ أَعْمَالَهُمْ

**“Enyi mlio amini! Mkimnusuru Mwenyezi Mungu naye atakunusuruni na ataithibitisha miguu yenu. Na walio kufuru, basi kwao ni maangamizo, na atavipoteza vitendo vyao. Hayo ni kwa sababu waliyachukia aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, basi akaviangusha vitendo vyao.”** [Surah Muhammad 47:7-9].

**H. 20 Jumada I 1445** **Hizb-ut-Tahrir**
**M. : Jumatatu, 04 Disemba 2023**

Afisi ya Habari Kitengo Cha Wanawake

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
HIZB UT TAHRIR

KUMB: 19/1445 Ijumaa, 09 Jumada II 1445 H 22/12/2023 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# "Je, Palestina Tutaikomboa Vipi?"

# Kongamano la Kimataifa la Wanawake Mtandaoni juu ya Palestina Lililoandaliwa na Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir kwa Ushirikiano na Wanawake wa Hizb ut Tahrir Ulimwenguni

Huku mauaji ya halaiki na mzingiro wa kikatili juu ya Gaza yakiendelea, na ugaidi, kukamatwa kwa watu wengi na mauaji ya Wapalestina katika Ukingo wa Magharibi yakipamba moto mikononi mwa umbile katili uaji la Kizayuni, miito imepazwa kote ulimwenguni, kutoka kwa Waislamu na vilevile wasiokuwa Waislamu, ya 'Ukombozi wa Palestina'. Hata hivyo, ufafanuzi unahitajika wa 'Ukombozi wa Palestina' inajumuisha nini kiuhalisia na jinsi ukombozi wa Palestina unaweza kupatikana kivitendo. Baadhi wanaendelea kuunga mkono lile linaloitwa suluhisho la dola mbili kumaliza umwagaji damu, huku wengine wakipigia debe uanzishwaji wa dola moja kwa msingi wa kanuni za kisekula za kidemokrasia ambapo Waislamu, Mayahudi na Wakristo watagawanya mamlaka ya kisiasa.

Pia kumekuwa na miito ya kulisusia umbile la Kizayuni na kampuni zinazoliunga mkono, na pia kukoleza shinikizo kwa serikali kuulazimisha uvamizi wa mauaji ya halaiki kukomesha mauaji yake ya watu wengi na kukubali kusitisha mapigano. Pamoja na hayo, kumekuwa na wito wenye nguvu unaotoka kwa Waislamu kote ulimwenguni wa ukombozi wa Ardhi nzima Iliyobarikiwa ya Palestina kwa kuhamasisha majeshi ya Waislamu kupitia usimamishaji wa uongozi wa mfumo na dola ya Kiislamu - Khilafah kwa njia ya Utume. Hivyo ni ipi njia na mbinu ya kweli ya 'Ukombozi wa Palestina'?

Mnamo Jumamosi Disemba 30, Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir kwa ushirikiano na Wanawake wa Hizb ut Tahrir ulimwenguni kitaandaa Kongamano la Kimataifa la Wanawake la Mtandaoni juu ya Palestina kujibu swali hili kwa undani. Amali hii itajumuisha wanapaneli wa kike kutoka Palestina, Uturuki, Tunisia, Indonesia, Amerika na Uingereza.

Kongamano hili litachunguza kwa undani mapendekezo na masuluhisho mbali mbali yanazowasilishwa kukomesha mauaji ya halaiki ya Gaza na kuleta haki na ulinzi kwa Waislamu wa Palestina. Litahoji dori na umuhimu wa Umoja wa Mataifa na Mfumo wa Kilimwengu wa Kimataifa katika kuzuia mauwaji wa kimbari ya Wapalestina kutoka ardhi yao. Litashughulikia vizuizi vikuu vyenye kuzuia ukombozi wa Palestina na ambavyo vinawezesha uendeleaji wa uhalifu wa umbile la Kizayuni. Na litauliza ni kwa nini serikali za ardhi za Waislamu zimeshindwa kutumia nguvu na ushawishi wa kiuchumi, kisiasa, kimkakati na kijeshi kuwalinda Waislamu wa Palestina kutokana na uvamizi huu wa kikatili na kusaidia ukombozi wa Ardhi hii Iliyobarikiwa. La muhimu, kongamano hili litashughulikia suluhisho la Kiislamu, la kivitendo na la kudumu kwa ukaliwaji kimabavu wa Palestina, na dori ya Ummah wa Kiislamu, watu wao wenye ushawishi, wanazuoni na majeshi yao katika kukomesha umwagaji damu huu. Pia litahoji iwapo uhamasishaji wa majeshi ya Waislamu kuikomboa Ardhi nzima ya Palestina kutokana na ukaliwaji kimabavu wa Wazayuni ni lengo la kihakika, na ikiwa ni hivyo - vipi linaweza kupatikana. Kwa kuongezea, amali hii itajadili jinsi amani na usalama kwa Waislamu, Wakristo, Mayahudi na wale wa imani zote inaweza kupatikana tu eneo hilo kupitia kurudi kwa utawala wa Kiislamu wa dola ya Khilafah ambayo inafurahia urithi wa kihistoria wenye kuhakikisha haki za watu wa imani zote, jamii na makabila chini ya mfumo wake zilihakikishwa na kulindwa. Wanapaneli pia watatoa ufahamu juu ya fikra, mhemko na wito wa umma, watu wenye ushawishi na majeshi ndani ya eneo lao dhidi ya uvamizi wa Palestina.

Tunatumai Bi idhnillah kwamba kongamano hili litafafanua njia wazi ya ukombozi wa Palestina ili kukomesha kiwango kisichoelezeka cha mateso, maumivu, dhulma na udhalilishaji wanaopitia ndugu na dada zetu kwa zaidi ya miongo saba ya giza. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

وَإِنِ اسْتَنصَرُوكُمْ فِي الدِّينِ فَعَلَيْكُمُ النَّصْرُ

**"Lakini wakiomba msaada kwenu katika Dini, basi ni juu yenu kuwasaidia."** [Al-Anfaal 8:72]?

Kongamano hili ni HAFLA YA WANAWAKE PEKEE na litakuwa kwa Kiingereza. Litafanyika 12:30pm GMT (3:30pm Saa za Madina). Kwa maelezo zaidi au ili kuhudhuria kongamano hili, tafadhali wasiliana na anwani ifuatayo:

FreePalestineConf@gmail.com

**Dkt. Nazreen Nawaz**
**Mkurugenzi wa Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Mzozo wa Gaza Wafichua Viwango Maradufu vya Wamagharibi




Mzozo wa Gaza unaoendelea ndani ya Ardhi ya Baraka ya Palestina ni baraka iliyojificha. Wamagharibi wakoloni wakiongozwa na Amerika na washirika wake wamefichuliwa kikamilifu. Hakika, upatilizaji wa matumizi ya viwango maradufu uko juu mno. Matukio yafuatayo ni baadhi tu yanayothibitisha hilo:

**Kwanza,** mnamo Machi 27, 2023, Baraza la Pili la Kabla-Kesi la Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) ilitoa hati za kukamatwa kwa Rais wa Urusi, Vladmir Putin na Kamishna wa Urusi wa Haki za Watoto, Maria Alekseyevna Lvova-Belova. Msingi wa maamuzi yao ni ripoti iliyoandaliwa na watafiti wa Chuo Kikuu cha Yale waliodhaminiwa na Kitengo cha Wizara ya Kigeni cha Amerika, iliyodai kwamba Urusi iliwahamisha kinyume cha sheria watoto zaidi ya 6,000 na kuwapeleka katika mtandao wa kambi ndani ya mipaka ya Urusi. Kwa upande mwingine, Waziri Mkuu, Benjamin Netanyahu anaendelea kuua zaidi ya watoto 10,000 ndani ya Ardhi ya Baraka ya Palestina. Hakujatolewa hati za kukamatwa kwake!

**Pili,** mnamo Juni 17, 2020, Rais wa Amerika, Donald Trump alisaini kuwa sheria Kifungu cha 2020 cha Sera za Haki za Kibinadamu kwa Uyghur. Sheria hiyo iliwawekea vikwazo maafisa wa Uchina wanaohusika na sera dhidi ya Uyghur. Kwa upande mwingine, Amerika na washirika wake hivi sasa wanatoa silaha na ulinzi kwa Umbile la Kiyahudi 'Israeli' dhidi ya Uislamu na Waislamu!

**Tatu,** ile inayojiita jamii ya kimataifa inailani Urusi kwa kukalia mipaka ya Ukraine. Ikidai kwamba Urusi haiheshimu sheria ya kimataifa ambayo yatambua mipaka ya Ukraine. Kwa upande mwingine, Amerika hivi sasa inahifadhi Azimio la Balfour la Uingereza ambalo ndio msingi unaotumiwa na Umbile la Kiyahudi 'Israeli' kuvamia na kumwaga damu za Waislamu na kunajisi matukufu ya Uislamu. Wakati huo huo, Mazayuni wanadai suluhisho la dola-moja. Amerika inawaunga mkono kwa kisingizio cha suluhisho la dola-mbili!

**Nne,** mnamo Disemba 5, 2023, kasuku 'vyombo vya habari' wa Kimagharibi wakiongozwa na muendeshaji kipindi kinachojiita Piers Morgan Uncensored, walikitumia kudhilalisha na kukejeli Uislamu na Waislamu. Hiyo ni kuhusiana na kuwa Waislamu duniani kote ikijumuisha Uingereza wakiongozwa na Hizb ut Tahrir waliandaa maandamano wakitaka kuunganishwa kwa majeshi ya Waislamu ili kuikomboa Gaza na Ardhi ya Baraka ya Palestina yote! Walimbandikizia mgeni katika kipindi hicho, kaka yetu Dkt. Abdul Wahid, Mwenyekiti wa sasa, Kamati ya Hizb ut Tahrir Uingereza kuwa ana msimamo mkali na anapigia debe Ugaidi! Badala ya muendeshaji kipindi, kukemea na kumshambulia mvamizi na muuaji, Umbile la Kiyahudi 'Israeli'!

**Tano,** mnamo Disemba 8, 2023, Amerika ilipiga kura ya turufu dhidi ya pendekezo la Umoja wa Mataifa kwamba mzozo usitishwe ndani ya Gaza!

**Sita,** mnamo Disemba 13, 2023, watawala Waislamu vibaraka wa wakoloni waliamrishwa na mabwana zao wakoloni Wamagharibi kufanya mkutano wa pili mjini Riyadh, Saudi Arabia kuwaleta pamoja Waislamu wakuu wa majeshi chini ya mwamvuli wa Muungano wa

***Endelea... UK 6***

Kiislamu wa Kijeshi wa Kupambana na Ugaidi (IMCTC) uliobuniwa mnano Disemba 2015 na utawala wa Saudi uliolaaniwa na uliojaa hila ukiongozwa na Mohamed bin Salman. Ajenda kuu ilikuwa ni kutathmini mkakati na kufaulu kwa muungano kuhusiana na kutatua masuala ya kimfumo, kimawasiliano, kifedha na oparesheni za kijeshi za makundi ya kigaidi kwa mujibu wa maamrisho ya Wamagharibi ambayo yanajumuisha Hamas!

**Saba,** mnamo Disemba 19, 2023, Amerika ilitangaza muungano wa mataifa 10 unaoitwa Oparesheni ya Ulinzi wa Ustawi, ili kuweza kulinda meli zinazotumia Bahari Nyekundu kutokamana na mashambulizi ya Houth yanayolenga vyombo vinavyomilikiwa na Umbile la Kiyahudi 'Israeli' au kutoka nchi zinazoliunga mkono kwa njia ya moja kwa moja au isiyokuwa hiyo! Hakika, kuna ustawi katika kulinda muuaji wa Waislamu!

**Nane,** kuwashika na kuwanyamazisha Waislamu wakijumuisha wanachuoni ndani ya ulimwengu wa Waislamu. Mfano wa hivi majuzi ni ule wa utawala wa Saudi Arabia, kumshika Muislamu mwanamume katika Msikiti wa Mtume ndani ya Madinah, kwa kosa tu la kuomba dua kwa ajili ya ukombozi wa Qiblah cha Kwanza cha Waislamu, Masjid al-Aqsa na Ardhi ya Baraka ya Palestina yote! Wanachuoni waovu ndani ya Saudi Arabia na nchi nyingine za Waislamu wako kimya kabisa kama ambaye yanayotokea Gaza hayawahusu. Kufanya mambo kuwa mabaya zaidi, wanashughulika nyuma ya pazia kuhalalisha mahusiano na muuaji wa Waislamu na kunajisi matukufu ya Uislamu! Aibu iliyoje!

Hayo hapo juu ni baadhi tu ya mifano inayothibitisha kuanguka kwa mfumo wa Kimagharibi uliofeli na uliojaa uhadaifu na wafuasi wake popote walipo. Kwa mara nyingine Wamagharibi wakoloni wamefichuliwa na hawana popote pakuficha sura zao. Walikuwa wakijipiga kifua kuwa wao ndio ngome ya demokrasia, walinzi wa haki za kibinadamu, wanaoheshimu sheria za kimataifa nk. Hakika, wao sio chochote, bali ni mabwana katika udanganyifu wa kisiasa, kijamii na kiuchumi!

Wamagharibi na wapambe wao wamepanua upatilizaji wa watu kwa sharti itawafikisha katika maslahi yao ima ya kindani au ng'ambo. Mfano mzuri ni Kenya, katika miaka ya 1950 Waingereza waliwabandikiza wapiganaji wa Mau Mau wakweli kuwa ni magaidi na yeyote aliyewahurumia yuko pamoja nao. Hivyo basi, wakawashika, wakawatesa na kuwaua kwa kudai uhuru! Hivi majuzi, Amerika chini ya utawala wa Biden, waliwabandikiza wale wanaojiita Weupe watukufu kuwa ni magaidi! Kwa kuongezea, polisi nchini India mnamo Novemba 28, 2023 waliwabandikiza wanafunzi saba kutoka Kashmir kuwa magaidi na kuwashika, kwa kosa tu la kusherehekea Australia kuishinda timu ya kriketi ya India!

Kila kitu sasa kiko wazi kama ilivyo nyeusi na nyeupe. Kila mtu anaweza kujionea mwenyewe na kuwa hakimu.

Matukio ya kimataifa yanawafungua macho wale ambao wameisoma historia kwa makini na kuweza kuunganisha vitone. Ubwana wa Amerika unakaribia kutangazwa kuwa umekufa na nafasi yake kuchukuliwa SIO na Uchina au ule unaoitwa muungano wa BRICS+ kwa sura ya ulimwengu wa wenye usemi wengi! Badala yake ni kuwa nafasi yake itakaliwa na kurudishwa tena maisha ya Kiislamu kupitia kuisimamisha Serikali ya Kiislamu, Khilafah kwa njia ya Utume. Njama zote ovu dhidi ya kuchelewesha kuchipuza Khilafah, zimefeli, kuanzia na ile ya kubuni kijidude kwa jina ISIS, kuubandikiza Uislamu kuwa ni mfumo wa siasa kali na Waislamu kuwa watu wenye misimamo mikali!

Wakati ni ndio huu kwa Waislamu hususan walioko ndani ya majeshi ya Waislamu kuweza kunyanyuka na kuitikia mwito kutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt): يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ اسْتَجِيبُواْ لِلّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُم لِمَا يُحْيِيكُمْ وَاعْلَمُواْ أَنَّ اللّهَ يَحُولُ بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَلْبِهِ وَأَنَّهُ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ **"Enyi mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu huingia kati ya mtu na moyo wake, na kwamba hakika kwake Yeye tu mtakusanywa."** [Al-Anfal: 24]. Kwa kuongezea, jamaa za wanajeshi lazima wapatilize fursa kuwakumbusha jamaa zao kwamba kutoa msaada (nusrah) kwa maana kuitikia mwito wa Mwenyezi Mungu (swt) ni wajibu ambao kwamba lau Hautatekelezwa utawapelekea kulaaniwa na Mwenyezi Mungu (swt)! Njia ni mbili, ima ni wanajeshi kujibu mwito wa Mwenyezi Mungu (swt) au kuendelea kubakia wametiwa minyororo ndani ya kambi zao za kijeshi. Wakisubiri maagizo kutoka kwa watawala Waislamu vibaraka wa wakoloni, ambao wao wenyewe wanasubiri maagizo kutoka Washington, London, Paris, Berlin, Beijing na Moscow!

Ama kuhusu Waislamu waliobakia ndani ya Ummah hususan wale walioko ndani ya nchi za Waislamu, lazima wayaelekeze maandamano yao na hasira zao katika nyumba (ikulu) za watawala Waislamu vibaraka wa wakoloni. Fauka ya hayo, wamtake ajifunge na atekeleze kwa ukamilifu Shari'ah ya Kiislamu. Agizo lake la kwanza liwe ni kwa majeshi kuikomboa Ardhi ya Baraka ya Palestina. Kukosa kufanya hivyo, wampindue na nafasi yake kuchukuliwa na mwanamume Muislamu muadilifu, Khalifah. Inaonekana kuwa ni kazi ngumu mno kwa wale waliotekwa na fikra za kisekula za kirasilimali, lakini ni rahisi kutekeleza unapotekwa na uchajimungu (taqwa) na ukweli (ikhlass). Mwenyezi Mungu (swt) alisema:

وَيَوۡمَئِذٖ يَفۡرَحُ ٱلۡمُؤۡمِنُونَ

**"Na siku hiyo Waumini watafurahi."** [30. Ar-Rum: 4]

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Ali Nassoro (Abu Taqiuddin)**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

**Afisi ya Habari Uzbekistan**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

KUMB: 07/1445 | Alhamisi, 15 Jumada II 1445 H | 28/12/2023 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Tanzia ya Mwanachama wa Hizb ut Tahrir katika Gereza la China

Uhalifu mwingine mpya imeongezwa katika orodha ya ukatili unaofanywa na serikali ya China inayoendesha vita vikali dhidi ya Uislamu na Waislamu. Utawala wa China ulitangaza kifo cha Syed Jahan Muhammad Khanovich Nodirov kutoka Andijan, mwanachama wa Hizb ut Tahrir, mnamo Novemba 28, 2023. Syed Jahan, ambaye aliuawa shahidi katika gereza moja la Beijing, alikuwa mwanaharakati miongoni mwa ndugu zetu wa Uighur huko Turkestan Mashariki, akilingania kunyanyuliwa kwa neno la Mwenyezi Mungu. Alifungwa na serikali ya China katika msimu wa kiangazi wa mwaka 2000. Hata hivyo, hukumu hiyo ilisomwa baada ya miaka 19, na Syed Jahan alinyimwa uhuru wake kwa miaka 20, bila kuzingatia miaka mingi aliyokaa gerezani. Mkewe Muighur anasalia kuzuizini katika kambi ya mateso, mahali pa ukandamizaji na mateso. Jamaa zake wanasema kwamba Syed Jahan alisalia katika sehemu ya matibabu ya gereza la Beijing katika siku zake za mwisho.

Inafahamika kuwa China ambayo haina tofauti na Mayahudi katika uadui wake dhidi ya Uislamu na Waislamu inajihusisha na vitendo viovu vya ukandamizaji na mauaji ya kikatili dhidi ya Waislamu wa Turkestan Mashariki. Inawaweka mamilioni ya Waislamu katika kambi za uzuizi zinazojulikana kama "shule za ufutaji fikra" na inatumia mbinu za mateso ya kutisha dhidi yao. Leo, China inasubutu tu kuwashambulia Waislamu kwa sababu Waislamu hawana Khalifa ambaye angeweza kutumika kama ngao ya ulinzi. Serikali ya Mirziyoyev nchini Uzbekistan, kwa mfano, haiwalindi wana wa Umma huu; kinyume chake, inafanana na serikali ya China katika kutekeleza jinai dhidi ya Waislamu. Ndio maana utawala wa China unaendelea kufanya jinai za kutisha dhidi ya Waislamu bila ya wasi wasi wowote.

Mwamko wa Uislamu unakuja kupitia ushindi wa Mwenyezi Mungu Peke Yake, na mti huu wa ushindi na utukufu unanyweshwa kwa damu ya ndugu zetu mashahidi, kama Syed Jahan, ambaye alibeba mzigo wa ulinganizi huu wenye changamoto. Mashahidi wamechaguliwa na Mwenyezi Mungu mwenyewe. Kwa hakika wao ni wateule na waja wa karibu wa Mwenyezi Mungu. Pamoja na kuhuzunishwa na kuondokewa na ndugu yetu Syed Jahan hapa duniani, tunampongeza kwa sababu alifikia mwisho mwema wa maisha, ambao ni Shahada (kuuawa shahidi)! Kama Mwenyezi Mungu anavyosema:

مِّنَ الْمُؤْمِنِينَ رِجَالٌ صَدَقُوا مَا عَاهَدُوا اللَّهَ عَلَيْهِ فَمِنْهُم مَّن قَضَىٰ نَحْبَهُ وَمِنْهُم مَّن يَنتَظِرُ وَمَا بَدَّلُوا تَبْدِيلًا

**“Miongoni mwa Waumini wapo watu walio timiza waliyo ahidiana na Mwenyezi Mungu. Baadhi yao wamekwisha kufa, na baadhi wanangojea, wala hawakubadilisha (ahadi) hata kidogo.”** [Al-Ahzab:23].

Twamuomba Mwenyezi Mungu (swt), amuweke ndugu yetu Syed Jahan pamoja na ndugu zetu mashahidi wengine katika Jannah, miongoni mwa mitume, wakweli, mashahidi, na watu wema, na hawa ni maswahaba wema walioje. Hakika, tunamuomba Mwenyezi Mungu (swt) subra na kheri kwa familia yake na jamaa zake. Hakika, Khilafah Rashida, ambayo itarejea hivi karibuni kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, kwa hakika itawalipizia kisasi ndugu zetu waliodhulumiwa na mashahidi kama Syed Jahan, kutoka kwa serikali ya China na wakoloni wengine wa makafiri.

وَيَقُولُونَ مَتَى هَذَا الْفَتْحُ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ * قُلْ يَوْمَ الْفَتْحِ لَا يَنفَعُ الَّذِينَ كَفَرُوا إِيمَانُهُمْ وَلَا هُمْ يُنظَرُونَ

**“Wanasema: Ushindi huu ni lini, kama mnasema kweli? * Sema: Siku ya Ushindi, wale walio kufuru imani yao haitawafaa kitu, wala wao hawatapewa muhula.”** [As-Sajda:28-29]

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Uzbekistan**

# Gaza Yafunua na Kufichua



Katika wiki ndefu, zenye uchungu, tangu 7 Oktoba 2023, Gaza imefunua haki, na kufichua batili. Imebaini ukweli juu ya watu wa Gaza, Ummah wa Kiislamu kwa jumla, na wasio Waislamu wenye akili adilifu kote ulimwenguni. Imefichua uhalisia wa umbile la Kizayuni, dola za Magharibi zinazolisaidia na watawala wa Waislamu wanaoshirikiana. Kwa kufichua na kufunua, imetoa mwelekeo kwa Ummah wa Kiislamu na majeshi yake, juu ya kile ambacho kinapaswa kufanywa sasa.

**Gaza imefunua kheri katika watu wake.** Watu wake wana uvumilivu juu ya hasara kubwa. Wao ni shupavu usoni mwa uvamizi mkubwa. Hawalalamiki juu ya mitihani mizito. Wanatabasamu ili kuwapa wengine faraja, huku wao wenyewe wakiwa na maumivu. Wanagawiana chakula, katikati ya uhaba mkubwa na njaa. Wanainua mikono yao katika Dua ili kuwalipa fidia kwa hasara zao kubwa. Wameutikisa ulimwengu kwa Iman yao, wakijitahidi kupendwa na Mwenyezi Mungu (swt). Hakika, pindi Mwenyezi Mungu (swt) anapowapenda watu, Yeye (swt) huwapa mitihani. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema,

إِنَّ اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ إِذَا أَحَبَّ قَوْمًا ابْتَلَاهُمْ فَمَنْ صَبَرَ فَلَهُ الصَّبْرُ وَمَنْ جَزِعَ فَلَهُ الْجَزَعُ

**"Hakika pindi Mwenyezi Mungu (swt) anapowapenda watu huwapa mitihani. Basi mwenye kusubiri atalipwa ujira wa Subira, na mwenye kunung'unika atalipwa manung'uniko."** [Imepokewa na Ahmad kupitia Mahmud b. Labeed].

**Gaza amefichua kheri katika Ummah wa Kiislamu.** Waislamu hawana utulivu wana maumivu, kwa mateso ya watu wa Gaza. Wanafanya kila wanachoweza. Wanaomba dua, mpaka mikono yao inauma. Wanatoa misaada, wakizibakisha tupu nyumba zao. Wanamsusia adui, na kusababisha hasara kubwa. Wanaomba mipaka ifunguliwe, ili waweze kutuma vijana wao. Wanayataka majeshi yao kutaharaki. Hakika Waislamu ni mwili mmoja, uliounganishwa na Iman yao. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema,

تَرَى الْمُؤْمِنِينَ فِي تَرَاحُمِهِمْ وَتَوَادِّهِمْ وَتَعَاطُفِهِمْ كَمَثَلِ الْجَسَدِ إِذَا اشْتَكَى عُضْوًا
تَدَاعَى لَهُ سَائِرُ جَسَدِهِ بِالسَّهَرِ وَالْحُمَّى

**"Utawaona Waumini, katika kuhurumiana kwao na kupendana kwao na kuoneana upole kwao, ni mithili ya mwili mmoja. Pindi kiungo chochote kinaposhtakia maumivu, mwili wake mzima huitikia kwa kukosa usingizi na homa."**

**Gaza imefunua upokewaji wa Uislamu, miongoni mwa watu wenye akili adilifu wa ulimwengu.** Wengi wasiokuwa Waislamu wameonyesha hasira yao kwa dhulma dhidi ya watu wa Gaza. Wengi sasa wanatofautisha kati ya Uzayuni na Uyahudi. Wengi wameathirika na uvumilivu wa Waislamu wa Gaza. Baadhi yao wameanza kutafuta chanzo cha uvumilivu kama huo. Baadhi ya hawa wamesilimu, wakaribishwa kwa dhati na Ummah wa Kiislamu. Kukubaliwa huku kwa Uislamu ni katika wakati ambao hakuna dola inayotabikisha Uislamu. Vipi basi katika wakati ambapo Uislamu unatabikishwa na dola, na Uislamu unaonekana

*Endelea... UK 9*

katika utukufu wake kamili? Thauban ameripoti kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema, إِنَّ اللَّهَ زَوَى لِيَ الأَرْضَ فَرَأَيْتُ مَشَارِقَهَا وَمَغَارِبَهَا وَإِنَّ أُمَّتِي سَيَبْلُغُ مُلْكُهَا مَا زُوِيَ لِي مِنْهَا **"Hakika Mwenyezi Mungu alinikundulia mimi ardhi. Basi nikaiona mashariki yake na magharibi yake. Hakika ufalme wa Ummah wangu utafikia ncha hizo ambazo zilikunduliwa kwangu."** [Muslim].

**Gaza amelifichua umbile la Kizayuni, ukatili wake na uadui wake, na pia udhaifu na uoga wake.** Umbile la Kiyahudi halikuacha aina yoyote ya jinai pasi na kuitenda. Lililenga watoto kwa walengaji shabaha, kama ambavyo lililenga mahospitali kwa mabomu. Baadaye likaficha uhalifu wake kwa pazia la uongo na nyudhuru zilizotolewa na Marekani, lilianza kutekeleza uhalifu wake bila ya udhuru. Linaua kwa ukatili na udhalimu, likikosa kabisa "maadili" au "desturi" au "ubinadamu," ambayo wanadamu wameyazoea katika vita. Hakika, maneno ya Mwenyezi Mungu (swt) ni kweli kuhusu wao,

لَا يَرْقُبُونَ فِي مُؤْمِنٍ إِلًّا وَلَا ذِمَّةً ۚ وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُعْتَدُونَ

**"Hawatazami kwa Muumini udugu wala ahadi; basi hao ndio warukao mipaka."** [Surah At-Tawba 9:10]. Yote haya ni mbali na ukweli kwamba Gaza imefichua udhaifu wa vikosi vya ukaliaji kimabavu. Licha ya silaha zao za kisasa, vikosi vioga vya askari wa Kizayuni havikuweza kuvishinda vikundi vidogo vilivyo na silaha duni, mujahidina mashujaa. Vipi basi lau wangekabiliana na jeshi moja la Waislamu?

**Gaza imefichua serikali za Kimagharibi katika kuunga mkono kwa udhalimu wa Wazayuni.** Dola ya Kizayuni inatekeleza ukatili wake mbele ya macho ya Magharibi muongo na mnafiki. Kujitolea kwa Magharibi kwa haki za binadamu, haki za wanawake, haki za watoto na haki za wanyama kumefichuliwa wazi. Kwa kuongezea, umbile la Kiyahudi linawauwa Waislamu kwa ridhaa na idhini ya Marekani, na ushiriki wake changamfu na msaada, kupitia propaganda za vyombo vya habari, ufadhili na silaha. Ushiriki wa Marekani sio chini ya kura yake ya turufu dhidi ya azimio lililopendekezwa la Umoja wa Mataifa la kusitisha mapigano mnamo 8 Disemba 2023. Yote haya sio chini ya idhini ya Marekani ya suluhisho ovu la dola mbili. Ni mpango wa kikatili wa Marekani unaokusudia kuikabidhi sehemu kubwa ya Ardhi Iliyobarikiwa kwa wavamizi wachokozi, na kuliacha umbo lisilo na silaha na duni, chini ya pazia la "Dola ya Palestina." Hakika, serikali za Kimagharibi na umbile la Mayahudi ni kama Mwenyezi Mungu (swt) ilivyowasifu, pindi Yeye (swt) aliposema,

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْيَهُودَ وَالنَّصَارَى أَوْلِيَاءَ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ

**"Enyi mlio amini! Msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa ni marafiki. Wao ni marafiki wao kwa wao."** [Surah Al-Ma'ida:51].

**Gaza imefichua watawala wa Waislamu.** Hata wakati umbile la Mayahudi likilipua mahospitali na shule, serikali ya Jordan ilidumisha daraja lake la angani kwa umbile la Kiyahudi, likitoa vifaa muhimu vya Kimarekani. Imarati (UAE) ilitia saini makubaliano ya kuendesha daraja la ardhini, kati ya bandari za Dubai na Haifa, kupitia eneo la Saudia na Jordan, kwa lengo la kukiuka vitisho kwa njia za usafirishaji wa meli. Watawala wa Waislamu wanafanya hivyo, badala ya kukata bahari, ardhi, na anga za ulimwengu, kuzuia usambazaji wa mafuta, na kutumia nguvu zao zote kukomesha umwagaji damu, wakati wanao uwezo wa kufanya hivyo. Misri inadumisha kufunga Kivuko cha Rafah, licha ya jeshi lake kuwa tayari zaidi na uwezo wa kuwanusuru Waislamu wa Gaza. Ama watawala wa Pakistan na Uturuki, wanapeleka askari wao kote ulimwenguni kwa maslahi ya Washington, huku, wakizuia askari walio tayari na wenye uwezo kutokana na kuinusuru Gaza katika kipindi chake cha uhitaji mkubwa. Baada ya kuwaangusha Waislamu wa Gaza na Ummah wa Kiislamu, sasa wanafanya kazi kutekeleza khiyana nyengine, suluhisho la dola mbili la Marekani. Wanafanya haya yote ingawa Mwenyezi Mungu (swt) amesema,

إِنَّمَا يَنْهَاكُمْ اللَّهُ عَنْ الَّذِينَ قَاتَلُوكُمْ فِي الدِّينِ وَأَخْرَجُوكُمْ مِنْ دِيَارِكُمْ وَظَاهَرُوا عَلَى إِخْرَاجِكُمْ أَنْ تَوَلَّوْهُمْ وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ فَأُوْلَئِكَ هُمْ الظَّالِمُونَ

**"Hakika Mwenyezi Mungu anakukatazeni kufanya urafiki na wale walio kupigeni vita, na wakakutoeni makwenu, na wakasaidia katika kufukuzwa kwenu. Na wanao wafanya hao marafiki basi hao ndio madhaalimu."** [Surah Al-Mumtahina 60:9].

**Gaza imefunua na kufichua na imetimiza jukumu lake mbele ya Mwenyezi Mungu (swt).** Ni juu yetu kuhakikisha kuwa hatujafanya mapungufu kwetu. Imetuonyesha hali na njia ya kusonga mbele. Waislamu wa Gaza ni wema. Ummah wa Kiislamu unasonga kwenye Dini yake. Kuna kundi kubwa la wasiokuwa Waislamu ambao wanaweza kuona dhulma ya umbile la Kiyahudi na serikali za Kimagharibi zinazoliunga mkono, kwa upande mmoja, na misimamo mizuri ya Waislamu. Umbile la Mayahudi sio watu wanaoheshimu mikataba wala ahadi. Serikali za Kimagharibi ni zile zinazounga mkono umbile la Mayahudi katika vita vya wazi dhidi ya Waislamu. Watawala wa Waislamu ndio kikwazo pekee kwa majeshi kutaharaki kunusuru Uislamu na Waislamu. Mbele kuna njia moja pekee sasa. Ummah na majeshi yake lazima wawaondoe watawala wa Waislamu. Ni hapo ndipo Ummah wa Kiislamu unaweza kulazimisha kurudi nyuma kwa maadui zake kutoka kwa ardhi zake. Kwa hivyo, hebu Ummah na uyatake majeshi yake yaipe Hizb ut Tahrir Nusrah yao kwa ajili ya Khilafah kwa Njia ya Utume. Hebu uharibifu wa Gaza na uwe sura ya mwisho ya giza tangu kuvunjwa kwa Khilafah 1924 M, 1342 H.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Musab Umair – Wilayah Pakistan**

# HABARI NA MAONI
# Ushindi Utapatikana tu kwa Kulitokomeza Umbile Vamizi la Kiyahudi Pekee na hivyo Kuikomboa Ardhi Hiyo



**Habari:**

Gazeti la 'The Guardian' liliripoti mnamo 24 Disemba 2023, "Kwa uchache watu 166 wameuwawa tangu Jumamosi, wizara ya afya katika eneo linalo endeshwa na Hamas ilisema, ikifikisha idadi ya waliouwawa hadi 20,424, ingawa maelfu zaidi wanaaminika kuzikwa chini ya vifusi. Wizara hiyo haitofautishi baina ya vifo vya raia na wanamgambo, lakini takriban 70% ya wale waliouwawa wanaaminika kuwa wanawake na Watoto.

**Maoni:**

Jumuia ya kimataifa ingali imetulia tuli ikitazama mauwaji yakifanywa dhidi ya watu wa Gaza. Inahesabu idadi ya mashahidi kwa maelfu, kana kwamba inafurahia hali hiyo. Watawala wa Waislamu wangali wako laini kwa dola ya Kiyahudi, huku ikiimaliza Gaza wakaazi wake. Askari wanyoofu katika majeshi wangali wana hamu ya kushambulia Mayahudi, lakini uongozi wao hauteteleki. Vyombo vya habari vingali vinaripoti jinai za Mayahudi mjini Gaza, kana kwamba ni mzozo ulio nchi ya mbali, nap engine katika sayari nyengine. Vinaripoti kana kwamba mzozo huu ni filamu ya kivita, ambayo mwisho wake wema utashinda uovu, kwa mshangao wa mabadiliko ya utunzi ya mwelekezi wa filamu!

Hebu watu na wasipuuze ukweli kwamba tunakabiliana na uhalisia mchungu hadharani, sio wa kubuni, wa kuigiza. Tofauti ya kiidadi na zana kati ya makundi mawili yanayopigana ni kubwa mno. Idadi zilizotajwa hapo juu za vifo zinatoa Ushahidi kiwango kisicholingana cha hasara kati ya pande hizo mbili. Ikiwa Umma wa Kiislamu hautahamasika na majeshi yake yote, au hata baadhi yao, kuwanusuru watu wake mjini Gaza, idadi hizi zitaongezeka pakubwa, ilhali yale yaliyofichwa ni makubwa zaidi.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) aliwaadhibu Mayahudi waliokiuka mkataba wao katika Vita vya Khandaq, kwa kupitisha hukmu ya Saad bin Muadh juu yao. Yeye (saw) alimwambia Saad, إِنَّ هَؤُلَاءِ نَزَلُوا عَلَى حُكْمِكَ **"Watu hawa wamejisalimisha kwa hukmu yako"** Kwa hivyo Saad akasema, فإني أحكم فيهم أن تُقتل مقاتلتهم، وتسبى ذراريهم، وتقسَّم أموالهم **"Basi hakika hukmu yangu kwao ni wauwawe wapiganaji wao, kizazi chao kichukuliwe mateka, na mali yao igawanywe."** Kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) akasema, لَقَدْ حَكَمْتَ فِيهِمْ بِحُكْمِ اللَّهِ مِنْ فَوْقِ سَبْعِ سَمَاوَاتٍ **"Hakika umewahukumu kwa hukmu ya Mwenyezi Mungu aliye juu ya mbingu saba."**

Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) aliamuru wachimbiwe mashimo katika soko la Madina. Kisha yeye (saw) akatuma waletwe na wakaletwa. Shingo zao zikakatwa

***Endelea... UK 11***

ndani ya mashimo hayo, na wakatupwa humo. Wanaume waliouwawa walikuwa mia nne, takriban. Katika riwaya ya Ibn Ishaq katika Seerah, walikuwa wanaume mia saba.

Mwenyezi Mungu (swt) aliteremsha haya kuhusu wao,

وَأَنْزَلَ الَّذِينَ ظَاهَرُوهُمْ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ مِنْ صَيَاصِيهِمْ وَقَذَفَ فِي قُلُوبِهِمُ الرُّعْبَ فَرِيقًا تَقْتُلُونَ وَتَأْسِرُونَ فَرِيقًا

**"Na akawateremsha wale walio wasaidia (maadui) katika Watu wa Kitabu kutoka katika ngome zao; na akatia khofu katika nyoyo zao. Baadhi yao mkawa mnawauwa, na wengine mnawateka."** [Surah Al-Ahzab 33:26]. Mayahudi walistahili adhabu hii, ingawa hawakushiriki vitani dhidi ya Waislamu. Badala yake, waliwaruhusu washirika kufika Madina kupitia sehemu yao. Hii ndiyo dori ambayo serikali zinazoizunguka Palestina, Misri, Jordan, Uturuki na Imarati, zinaicheza leo, kwa kuwasaidia Mayahudi. Sasa je, ni ipi adhabu kwa wale wanaowauwa Waislamu? Utukufu wad amu ya Muislamu ni kubwa zaidi kuliko utukufu wa Al-Kaab Tukufu. Ikiwa kumuua Muislamu mmoja ni jambo kubwa sana, kuliko kuuwa maelfu ya wahalifu wa Kiyahudi, vipi basi wakati maelfu yetu wanauwawa?!

Matokeo yoyote ya vita hivi ambayo hayapelekei katika kutabikisha hukmu iliyoidhinishwa na Wahyi, hayatachukuliwa kuwa ni ushindi. Hayatapoza nyoyo za waumini. Ukombozi hautapatikana mikononi mwa makundi ya mujahidina mjini Gaza, licha ujasiri na ushujaa. Dori ya imefungika na kulizuia jeshi la adui, ilhali nusra wanayoihitaji sana ni lazima itoke kwa majeshi ya ulimwengu wa Kiislamu. Majeshi ndiyo yenye uwezo wa kulishinda kikamilifu umbile la Kiyahudi, kuwauwa wapiganaji wake, wale wanaotoa huduma na wale wa akiba, na kuwafukuza wao na wale walio nyuma yao.

Isipokuwa nusra hii ije, janga hilo litapanuka, siku baada ya siku. Dhambi la damu hii tukufu linaning'inia shingoni mwa maaisa wanyoofu katika majeshi, na sio tu kwenye shingo za viongozi wa kisiasa na kijeshi katika ulimwengu wa Kiislamu. Hii ni kwa sababu viongozi hao washafanya uamuzi wao, na kujitolea kwa msimamo wao wa kuwasaidia Mayahudi dhidi ya Waislamu, licha ya dhambi la Abu Righal, Mwenyezi Mungu (swt) amwangamize.

Hivyo matumaini yanabakia yamewaambata wale wanyoofu, ambao hawakuwachukua mashetani kama washirika, kuwapindua viongozi hawa, na kuwabadilisha kwa kiongozi mwenye ikhlasi wa wale wanaofanya kazi kusimamisha Khilafah Rashida kwa Njia ya Utume. Ni Khilafah ndio itakayo waongoza kupigana na kuwauwa Mayahudi, ambao Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) ametueleza kuwahusu.


Wanyoofu hawa ndio wale ambao lazima waharakishe na kurekebisha hali yao kabla ya kifo kuwakimbilia wao, huku watu wakiyarushia mawe makaburi yao, kama walivyolirushia mawe kaburi la Abu Righal, na kama watakavyo yarushia mawe makaburi ya viongozi wa sasa. Mwenyezi Mungu (swt) amesema,

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا خُذُوا حِذْرَكُمْ فَانْفِرُوا ثُبَاتٍ أَوِ انْفِرُوا جَمِيعًا

**"Enyi mlio amini! Chukueni hadhari yenu! Na mtoke kwa vikosi au tokeni nyote pamoja!"** [Surah An-Nisaa 4:71].

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Bilal al-Muhajir – Wilayah Pakistan**


WOMEN'S GLOBAL DAY OF ACTION
FOR PALESTINE
26 November 2023
KENYA
MUKO WAPI MAJESHI KUTOKA NCHI ZA KIISLAMU?
NOVEMBA 26
WHERE ARE THE ARMIES FROM MUSLIM COUNTRIES?
#ArmiesToAqsa
WOMEN'S GLOBAL DAY OF ACTION FOR PALESTINE
#ArmiesToAqsa
WOMENSCMOHT
WOMENFORKHILAFA
WOMENSHARIAH5


WOMEN'S GLOBAL DAY OF ACTION
FOR PALESTINE
26 November 2023
TURKIYE
WOMEN'S GLOBAL DAY OF ACTION FOR PALESTINE
#ArmiesToAqsa
WOMENSCMOHT
WOMENFORKHILAFA
WOMENSHARIAH5


WOMEN'S GLOBAL DAY OF ACTION
FOR PALESTINE
26 November 2023
BRITAIN
Women's Global Day of Action for PALESTINE
WOMEN'S GLOBAL DAY OF ACTION FOR PALESTINE
#ArmiesToAqsa
WOMENSCMOHT
WOMENFORKHILAFA
WOMENSHARIAH5


WOMEN'S GLOBAL DAY OF ACTION
FOR PALESTINE
26 November 2023
INDONESIA
WOMEN'S GLOBAL DAY OF ACTION FOR PALESTINE
#ArmiesToAqsa
WOMENSCMOHT
WOMENFORKHILAFA
WOMENSHARIAH5


WOMEN'S GLOBAL DAY OF ACTION
FOR PALESTINE
26 November 2023
BELGIUM
"O Muslim commanders! Do you not aspire to be remembered eternally like Salahuddin Al-Ayyubi? Become the heroes of the Ummah!"
WOMEN'S GLOBAL DAY OF ACTION FOR PALESTINE
#ArmiesToAqsa
WOMENSCMOHT
WOMENFORKHILAFA
WOMENSHARIAH5


WOMEN'S GLOBAL DAY OF ACTION
FOR PALESTINE
26 November 2023
AMERICA
WE ARE MOTHERS
WE ARE WIVES
OUR ARMIES SLEEP
WHILE GAZA
CRIES
THE MUSLIM IS THE BROTHER OF ANOTHER MUSLIM
MUSLIM ARMIES
LIBERATE PALESTINE
PALESTINE AWAITS ITS LIBERATORS
WOMEN'S GLOBAL DAY OF ACTION FOR PALESTINE
#ArmiesToAqsa
WOMENSCMOHT
WOMENFORKHILAFA
WOMENSHARIAH5